# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land – A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE SIX: “A Continent So Near, Yet So Far”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI:Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: SULE AND FARAHANI WATCHING THE NEWS**

- **Farahani (m, 19)**
- **Sule (m, 19)**
- **Presenter (f, 30)**

**SCENE TWO: MARAGA FAMILY AT HOME AFTER SUPPER**

- **Mr. Maraga (m, 60)**
- **Mrs. Maraga (m, 55)**

**SCENE THREE: LINDA AND CHIVASI TALKING ONLINE**

- **Linda (f, 20)**
- **Chivasi (m, 22)**

**SCENE FOUR: LINDA CALLS FLORENCE FROM PHONE BOOTH**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**

**INTRO:**

Hujambo na kwa mara nyingine karibu kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio Noa Bongo jenga maisha yako. Hii ni sehemu ya sita katika tamthlia **“Ardhi ya Ahadi- kuhusu Waafrica wanaohamia Ulaya**.” Kukumbusha tu, katika kipindi kichotangulia Linda anawasili Ulaya baada ya safari inayokumbwa na panda shuka nyingi, na sasa anajianda kuanza masomo yake katika chuo kikuu. Kwa upande mwengine Farahani anarejeshwa Afrika baada ya kuvuka kutaka kuingia Ulaya bila vibali halisi vya usafiri. Nini kitakachotokea leo. Endelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi hiki **Bara lililokaribu sana japo Mbali.** Basi katika kipindi hiki tunaanzia huko Africa Kaskazini ambako tunakutana na Farahali na rafiki yake Sule wakitazama Televisheni. Farahani haamini macho yake anapojiona kwenye habari. Ripoti hiyo inahusu mashua moja iliyonaswa ikiwa na wahamiaji wanaojaribu kuvuka na kuingia Ulaya bila vibali halisi vya usafiri. Bado Farahali hajamdokezea mtu yoyote kuhusu kisa hicho, hata rafiki yake Sule…!

**SCENE ONE: SULE AND FARAHANI WATCHING NEWS**

1. **SFX: JINGLE PLAYS, SIGNALLING BREAKING NEWS ON TV**

2. **PRESENTER:** Hujambo na karibu kwenye mkusanyiko wa habari zetu wiki hii. Wahamiaji hawa baadhi yao kutoka Jamhuri ya Afrika ya Kati, walikamatwa siku ya

Jumatatu na maafisa wa usalama wa Ulaya wanaoshika doria Baharini, wakijaribu kuvuka na kuingia Ulaya bila hati halali za usafiri.Tunaarifiwa kwamba baadhi ya wahamiaji hao yaaminika walifariki wakiwa njiani kutokana na ukosefu wa maji mwilini. Wakati mashua hiyo ilipotia nanga,Mhamiaji mmoja alijirusha baharini akijaribu kutoroka lakini aliokolewa na maafisa wa usalama.Mashua hiyo imerejeshwa Afrika ilikotoka. Hii ni kuambatana na mkataba uliotiwa sahihi hivi majuzi baina ya serikali yetu na Jumuiya ya Ulaya kwamba wote watakaopatikana wakiingia Ulaya bila hati halisi za usafiri watarejeshwa nyumbani. Tutazidi kuwaletea habari zaidi kadri matukio yanavyochipuka. Katika habari nyingine Rais amebuni mpango mpya wa kuimarisha Miundo msingi katika eneo la kusini mwa Nchi.

3. **SFX: SUDDEN CUT IN BETWEEN THE NEWS TO ORIENTAL MUSIC ON TV, AS WHEN SOMEONE SWITCHES THE CHANNEL. ORIENTAL MUSIC PLAYING IN BACKGROUND**

4. **SULE:** **(shocked)** Farahani,kwanini unabadilisha stesheni ! Yule Mtu tumemuona kwenye Habari mnafanana sana. Umemuona?

5. **FARAHANI:** **(coughing)** Eeehh, ..mimi … uuuuh**….** Sio kipofu au kiziwi. Ndiyo nilimuona!

6. **SULE:** Ni wewe? Na hata husemi! Ni nini sasa? Bado unamipango ya kuvuka kwa mashua kuingia Ulaya? Watakukamata na kukurejesha tena nyumbani, si unafahali hilo!

7. **FARAHANI:** **(angrily)** Kwa hiyo? Hata wakinirejesha nyumbani, bado nitajaribu tena bahati yangu, mpaka pale watakuja kufahamu sura yangu na juhudi zangu za kutaka kuingia Ulaya! Na hapo wataniruhusu!. Sule tulikuwa karibu sana! Imani ndiyo nguzo hapa rafiki yangu!

8. **SULE:** **(unsure)** Oh, kumbe? Na sasa utafanya nini endapo maafisa wa usalama baharini hawatakuwepo kukuokoa usizame baharini?

9. **FARAHANI:** Nitaogelea. Nitatumia ujuzi wangu wote kuogelea **(contemplating)** Ah… Ulaya ni karibu sana, lakini Mbali!

Farahani hajatikisika na tisho hilo la kunusurika kifo.Je bado atajaribu kuhatarisha maisha kuvuka tena bahari kuingia Ulaya? Hayo ni baadaye lakini kwanza twende moja kwa moja katika eneo la Kusini mwa Afrika kukutana na wazazi wa Linda ambao wanaendelea kupata vinywaji taratibu baada ya chakula cha jioni. Mzee Maraga tayari ameanza kushikwa na wasi wasi kuhusu binti yake huko Ulaya.

**SCENE TWO: MARAGA FAMILY AT HOME AFTER SUPPER**

**SFX: clinking of glasses, pouring liquid into glasses, with evening atmo from outside (crickets)**

10. **MRS. MARAGA:** **(sipping her drink)** Wewe una wasi wasi sana. Hii itakuathiri afya yako. Linda amesema yuko salama. Hakikisho la kutuliza mioyo yetu.

11. **MR. MARAGA:** **(worried)**Hapana…alisikika matatizo! Namfahamu vyema binti yangu. Na huyu rafiki yake aliyemtaja ni nani? Ni siku yake ya kwanza huko Ulaya na tayari amefanya urafiki?

12. **MRS. MARAGA:** Linda ni Mtu anayependa kutangamana na watu.Kisha usisahau ni mrembo! Si ajabu kuanza urafiki haraka hivyo

13. **MR. MARAGA:** **(annoyed)** Wewe hunielewi? Binti yetu amekwenda Ulaya kusoma na sio kutafuta urafiki! Tayari ana marafiki wengi sana hapa nyumbani.

14. **MRS. MARAGA:** Ni sawa Mpenzi, nimekuelewa sasa! Lakini ninachomaanisha ni kwamba, Linda si Mtoto tena! Amekuwa mtu mzima kujua jambo baya na zuri. Na anafahamu vyema wajibu wake!

15. **MR. MARAGA :** Nina shaka sana kwamba huenda mambo si mazuri kwake. Hatungempeleka Ulaya. Yeye mwenyewe hakuwa tayari kwenda Ulaya. Kisha miaka mitatu!

Atawezaje kujimudu muda wote huo? Na je akiugua? Nani atamuuguza? Nitajilaumu sana.

**16. MRS. MARAGA:** Usijali,,wacha kufikiria hayo mume wangu. Msichana wetu yuko salama. Hii ni siku yake ya kwanza katika nchi ya kigeni, lazima atajisikia mnyonge tu! Anahitaji muda kuzoea maisha hayo ya Ulaya. Kwanini unakata tama mapema hivi Mume wangu, baada ya kujitolea kumpeleka huko?

**17. MR. MARAGA:** Moyo wangu utatua ikiwa nitazungumza naye tena.Hali ya mawasiliano hayakuwa mazuri wakati ule sikuweza kumsikia vizuri.

**18. MRS. MARAGA:** Sawa. Basi subiri tutazungumza naye tena, lakini mpe muda kwanza,usiwe na shaka. Usijitie ugonjwa wa moyo! Nadhani pia hujamwambia kwamba hatuna pesa za kutosha kumlipia karo yake miaka mwili ijayo?

**19. MR. MARAGA:** Bado sijamueleza. Ningewezaje kumwambia? Lakini yeye ni msichana mwerevu. Bila shaka atatafuta njia kugharamia masomo yake. Pindi akianza masomo tu atamaliza.

**20. NARRATOR**: Ni kweli Linda anapenda sana kusomea Sheria ya kimataifa, lakini Mamake anakosea anaposema kwamba atazoea maisha ya Ulaya. Miezi minne ya

kwanza haijakuwa rahisi kwa Linda. Isitoshe pesa za matumizi zimeanza kumuishia na tayari msimu wa baridi umengia. Anahitaji mavazi ya kujikinga baridi,koti la baridi katika vyumba vya wanafunzi. Sasa tujiunge na Linda akiwa kwenye mtandao wa Intaneti akiwasiliana na mchumba wake Chivasi.

**SCENE THREE: LINDA AND CHIVASI TALKING ONLINE**

**(In this dialogue there are background typing sfx every time Linda and Chivasi speak, as if chatting and reading out loud what they're typing)**

**21. SFX: TYPING ON COMPUTER KEYBOARD**

**22. CHIVASI:** **(reads out what he is typing)** Hello, Sema mke wangu mtarajiwa.… **(giggles)**

**23. LINDA:** **(reads out as she replies)** Hello, Mume wangu mtarajiwa… **(chuckles)**

**24. CHIVASI:** Waendeleaje na masomo? Na maisha ya wazungu huko Ulaya?

**25. LINDA:** Naendelea vizuri na masomo na wazungu nao hawana neno. Na wewe Je unaendeleaje?

**26. CHIVASI:** Sina raha! Nakutamani sana. Yaani hii miezi mine imekuwa kama miaka mine kwangu. Hatahivyo,

habari njema ni kwamba nimepata kazi, kama mhandisi mdogo.

**27. LINDA:** Pongezi, mpenzi,! Nafurahi kusikia habari hizo njema. Kisha wana wanasema hakuna kazi huko nyumbani?

**28. CHIVASI:** Kweli kunatatizo la ajira. Lazima uwe umehitimu vyema. Mimi nilikuwa na bahati sana!

**29. LINDA:** Hapana si bahati unastahili kwa kazi hiyo

**30. CHIVASI:** Vipi na hali yako ya kifedha? Unahitaji msaada wowote wa kifedha? Naelewa maisha ya Ulaya ni ghali mno, hasa kwa wanafunzi.

**31. LINDA:** Hapana. Sihitaji msada wowote wa kifedha kwa sasa. Naendelea vizuri tu. Tayari wewe mwenyewe una jukumu kubwa.

**32. CHIVASI:** Sawa lakini ukiwa na shida usisite kunieleza **(mockingly)** Afrika inaweza kutuma pesa Ulaya pia!

**33. LINDA:** **(laughs out loud)** Lo, Wachekesha. Kwaheri inabidi niondoke sasa sahamani sana Chivasi.

**34. CHIVASI:** **(pleading)** Mara moja hii? Naweza kukuona kidogo

tu kwa webcam? Ni miezi minne sasa …

**35. LINDA** **S**amahani mpenzi. sina cam katika komputa hii. Usiwe na haraka subira huvuta kheri. Kwaheri tutazungumza kesho. Nakupenda!

**36. CHIVASI:** **(sadly)** Hata mimi pia nakupenda. Kwaheri!

**37. SFX: LOGGING OUT OF AN ONLINE CHATTING WEBSITE**

**38. NARRATOR:** Linda anaondoka mtandaoni huku akiinamisha uso wake kwa aibu. Amemdanganya mpenzi anayetaka kufunga naye ndoa. Ukweli ni kwamba anahitaji msaada wa kifedha, pili hakuna mahali anakokwenda, na tatu komputa aliyokuwa akitumia ilikuwa na teknolojia ya Webcam. Baada ya kutangamana na wanafunzi wenzake kutoka Afrika, anafahamu kwamba wahamiaji wote hawapendi kuzungumzia matatizo yao. Sasa ameanza kuelewa alichokuwa akisema Florence, kwamba usiwaeleze ukweli watu wa nyumbani. Baada ya Linda kuondoka kwenye komputa yake anaenda moja kwa moja hadi kibanda cha simu kumpigia simu Florence.

**<u>SCENE THREE: LINDA CALLS FLORENCE FROM PHONE BOOTH</u>**

**39. SFX: DIALLING NUMBERS - 'BEEP' SOUND FROM TELEPHONE BOOTH**

**40. FLORENCE:** **(answers call)** Hello, Ni Florence hapa.

**41. LINDA:** **(sorrowful)** Habari Flo?...Ni Linda hapa... Unanikumbuka?

**42. FLORENCE:** **(excited)** Ah! Linda. Yule mwanasheria wa kimataifa. Nitakusau vipi? Siwezi kukusahau? Una tatizo? Unasikika mnyonge.

**43. LINDA:** Hmm… sijui nianzie wapi! Huu ni mwezi wa nne tangu niingie Ulaya na nimejifunza mengi, lakini …Florence maisha hapa ni magumu sana. Naona wanafunzi wenzangu wakitoka nje kila wikiendi huku mimi nikiwa nimeganda chumbani mwangu. Nimekuwa mlinzi wa makaazi yetu. Wanakula nje, na wavaa vizuri, mimi ninavaa rinda moja tu tangu nilipowasili. Sina hata mavazi rasmi ya kujikinga na baridi.

**44. FLORENCE:** Kwani wazazi wako hawaja kutumia pesa za matumizi?

**45. LINDA:** Hawaja nitumia chochote. Kwanza hawana uwezo, ingawa hawajanieleza hilo! Najua wametumia akiba yao yote kugharamia masomo yangu hapa chuoni. Nimekuwa nikiwasiliana na …. **(hesitates) …n**a mchumba wangu pia amepata kazi. Lakini siwezi kumuomba anitumie fedha… ama unalifikiriaje suala hilo?

**46. FLORENCE:** Hakuna haja, yeye yuko Afrika Linda!. Watu huko nyumbani wanahitaji msaada zaidi kuliko hapa. Unafikiri ni kwanini nilikwambia usiwaeleze watu wa nyumbani ukweli wa shida zako?

**47. LINDA:** **(answers)** Kwa sababu watu nyumbani hawatakuamini. Hawatakuelewa!

**48. FLORENCE:** Kabisa! Watu nyumbani hawajali kama una pesa au la, una mahali pa kulala au unaishi barabarani, ilimradi tu uko Ulaya, wanaamini kuwa unaishi maisha mazuri! Linda, usijali! Mimi nitajaribu kukusaidia! Sahau kabisa mambo ya mchumba wako. Nitakupa pesa kidogo kununua nguo, vipodozi na mahitaji yako mengine madogo madogo. Tukutane baadaye. Kumbuka huku ni Ulaya! Na ni ndoto ya Waafrika wengi kuja huku.

**49. LINDA:** **(so happy)** Oh, Florence! Sijui nikwambie nini? Nimekushukuru sana kwa ukarimu wako. Sijui nikulipe vipi!

**50. FLORENCE:** Usijali Linda. Nipigie simu kesho ili tuweze kukutana!

**51. LINDA:** Kwaheri Flo!

**52. SFX: PHONE RECEIVER PLACED BACK ON THE CRADLE**

**OUTRO:**

Linda anakata simu na kutabasamu kwa mara ya kwanza kabisa tangu awasili Ulaya. Sio  tu kwa sababu Florence amemuahidi kumpa msada wa kifedha bali pia atapata fursa nyingine ya kukutana naye na kumpa ushauri jinsi anavyoweza kujipatia pesa zake mwenyewe. Je ni ushauri gani Florence atakao mpa Linda? Kumbuka- amemshauri Linda amsahau kabisa mchumba wake Chivasi. Je Linda atafuata ushauri huo?

Basi hadi hapo, ndo tunafika mwisho wa kipindi hiki. Tukutane kwa sehemu inayofuata tusikie yatakayojiri kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu Waafrifk wanaohamia Ulaya. Unaweza pia kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu wa : dw-.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.